OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
IDODI SHULE YA SEKONDARI

SHULE YA SEKONDARI IDODI,
S. L. PEKEE-IDODI,
IRINGA

NAMBA ZA SIMU;
MKUU WA SHULE
0717055845/0745055854.

JINA LA MWANAFUNZI…….
S.L.P……
…….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI IDODI MWAKA 2022.

1.0.UTANGULIZI

1.1. Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO** katika shule ya sekondari Idodi mwaka 2022, kwa Tahasusi za HGE, HKL na HGK
Shule ya sekondari Idodi ipo umbali wa km 80 magharibi mwa mji wa Iringa katika Halmashauri ya wilaya ya Iringa.
Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini, unapatikana **stendi ya mabasi ya Mlandege** kwa nauli ya Tsh 4500/= kupitia barabara ya kwenda Ruaha National Park. Sehemu ya kushukia ni **Kibao cha shule ya sekondari Idodi.**

1.2. Muhula wa masomo unaanza tarehe **Julay 2022** tarehe ya kuripoti ni **julay 2022** utakapofika hapa shuleni utakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii, pamoja na kufuata sheria za shule ambazo zimeandikwa kwenye maelezo haya ya kujiunga na shule.
Mwanafunzi anapaswa kuja na fomu hii ikiwa imejazwa sehemu zote.

2.0.**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

2.1. SARE YA SHULE

i) Suruali 2 za rangi ya kijivu (mpauko) na siyo za mitumba, suruali iwe na marinda mawili na kwa suruali iwe na mifuko 3, wa nyuma 1 .
ii) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba jozi moja vya kisigino kifupi, sandals na raizon haviruhusiwi.
iii) Shati rangi nyeupe mikono mifupi
iv) Soksi ndefu jozi 2 za rangi nyeusi na viatu vya michezo jozi moja

v) Sare ya kazi ni suruali ya dark blue kwa wavulana na T-shirt ya Kijivu yenye kola (form six)
vi) Sare ya michezo ziwe ni bukta au Tracksuit za kijani
vii) T-shirt ya shule (yenye nembo ya shule inapatikana shuleni) Tsh 10,000/=
viii) Sweta la rangi ya maruni (shingo iwe V)
ix) Tai ifanane na rangi ya suruali ya kijivu
x) Nywele ziwe fupi kwa wote
xii) Mkanda wa suruali wa ngozi rangi nyeusi.
xiii) Raba jozi moja ya michezo.

2.2. MWANAFUNZI ANAPORIPOTI AWE NA VITU VIFUATAVYO.

I. Ndoo mbili moja lita **10** na nyingine lita **20** zenye mifuniko.
II. Jembe moja lenye mpini
III. Fagio moja ya kukaushia maji (dryer)
IV. Mafaili mawili (spring file)
V. Rimu ya karatasi moja(kwa mwaka)
VI. Godoro futi 6 kwa $2^{1/2}$ Mto
VII. Shuka mbili (wavulana pink)
VIII. Chandarua
IX. Daftari (counter book) kuanzia 10
X. Kamusi ya kiingereza-kiingereza (**English-English Dictionary**)
XI. Scientific calculators kwa wanafunzi wa Uchumi (HGE)
XII. Vitabu vya kutosha kulingana na Tahasusi (mchepuo) uliopangiwa
XIII. Vifaa vya hisabati-Mkebe (Mathematical set)
XIV. Vyombo vya chakula (container)
XV. Tochi moja ya betri au ya sola itakayotumika kukiwa na tatizo la mwanga
XVI. Mahitaji mengine binafsi.
XVII. Result slip na copy/kivuli yake, Kivuli/copy ya cheti cha kuzaliwa

3.0 ADA NA MICHANGO MINGINE

- Ada kwa mwaka **70,000/=(35,000/=**kwa muhula.)
- Taaluma **22,000/=**
- Kitambulisho na picha **6,000/=**
- Ukarabati wa samani **15,000/=**
- Wapishi, walinzi na vibarua wengine **40,000/= (20,000/=** kwa muhula)
- Bima ya afya na huduma ya kwanza **10,000/=**
- Mitihani ya kujipima **(Mock) 20,000/=**
- Fedha ya tahadhari **5000** (Haitarudishwa)

Jumla ya ada na michango mingine kwa mwanafunzi ni shilingi 188,000/= (Muhula wa kwanza 133,000/= na 55,000/= tu muhula wa pili).

ZINGATIA

Michango yote pamoja na ada ziingizwe benki kwenye akaunti namba (60501100039) NMB jina Idodi sec school. Andika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya benki ya malipo (BPS) na uje nayo siku ya kuripoti. Hatupokei hatupokei fedha mkononi kwa vyovyote vile.

4.0 SHERIA ZA SHULE.

1. Mwanafunzi anapaswa kuwepo katika eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalum kutoka kwa mkuu wa shule kwa kujaza fomu maalumu.

2. Mwanafunzi anatakiwa avae sare rasmi ya shule muda wote wa muhula wa shule, isipokuwa muda wa kazi za mikono na michezo. Aidha nguo za nyumbani haziruhusiwi.

3. Lugha chafu, matusi, dharau, ugomvi, mapigano, na fitina kwa mwanafunzi ni mwiko kabisa.

4. Mwanafunzi lazima awahi popote anapotakiwa.

5. Mwanafunzi anapaswa kusimama anaposalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri pia awaheshimu.

6. Unywaji wa vileo, kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote ni mwiko kwa mwanafunzi.

7. Wizi wa aina yoyote ni mwiko na marufuku na kosa kubwa kwa mwanafunzi.

8. Uharibifu wa mali ya binafsi na umma pia ni kosa kubwa.

9. Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima, mtiifu na mwenye adabu wakati wote kwa kila mtu.Ukaidi na ubishi kwa walimu/viongozi wake ni marufuku. Aidha kukataa adhabu kwa makusudi ni mwiko. Aidha kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu ni marufuku.

10. Wageni wa wanafunzi wanaruhusiwa kuonanana nao, baada ya kujitabulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu, kwa siku ya jumamosi na jumapili.

11. Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa wakati akiwa bado mwanafunzi akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kuwa na uhusiano wa mapenzi awapo mwanafunzi.

12. Ni mwiko kwa mwanafunzi yeyote kwenda kwenye nyumba za walimu na kufanya kazi bila ruhusa ya pekee kutoka kwa mwalimu mlezi/matron/patron.

13. Ni marufuku kwa wasichana kuingia mabweni ya wavulana, pia wavulana kutembelea katika mabweni ya wasichana. Iwapo inabidi ruhusa ya pekee kutoka kwa mwalimu mlezi, matron patron itatolewa.

14. Mapambo, kufuga kucha,kufuga ndevu na nakshi za aina yoyote ni marufuku kwa mwanafunzi. Msuko wa nywele kwa mwanafunzi hauruhusiwi, vinginevyo nywele zikatwe zibaki fupi kwa kuchana kirahisi.Mitindo ya kunyoa kihuni kama vile pank, denge, kipala hairuhusiwi hapa shuleni.

15. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu akiwa ndani ya eneo la shule na vyote vinavyohusiana na simu kama vile line ya simu, chaja, betry ya simu nk.

4.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi, uvutaji bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Makosa ya jinai.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma nay a binafsi
7. Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa na za uzalendo.
8. Kutoa mimba, kuoa au kuolewa, kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
9. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
10. Kukataa adhabu
11. Utoro wa muda mrefu.
12. Kumiliki simu,chaji, pasi, jagi la umeme computer au laini ya simu ukiwa hapa shuleni.
13.Kufanya mikutano bila kibali kutoka kwa mwalimu wa malezi.
14.Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua kama kunywa sumu na n.k.
15. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

BAKARI MSANGI
MKUU WA SHULE.

MAWASILIANO ZAIDI
OFISI YA MAKAMU MKUU WA SHULE
0768858783, 0713314172, 0753007649
OFISI YA TAALUMA
0764962989, 0768817810, 0744028000
OFISI YA MALEZI
0765335593, 0756679726, 0755867167

Fomu Na -B-

TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano wakati wote awapo shuleni. **Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu**.

Jina la mwanafunzi …… Kidato……mchepuo..... Mwaka……
Anwani ya nyumbani (anayotumia)……Tarehe ya kuzaliwa……
Namba ya simu(ya nyumbani/ya mzazi)……Mtaa/Kijiji anachotoka…….Kata…….
Tarafa…….Wilaya……Mkoa……..shule ya msingi aliyosoma…….
Shule ya Sekondari atokayo…… Namba ya Mtihani ya Kidato cha Nne……
Anwani ya shule …… ….Matokeo yake ya kidato cha nne……
Dini yake ni ……[Mkristo, Mwislamu n.k.]Dhehebu lake ni…… Mkatoliki, Mlutheri,Suni n.k}
Sahihi …… Tarehe……...

NB. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili Dini akiwa shuleni.

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi…….. NAKUBALI / SIKUBALI nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Idodi. Naahidi kuwa nitazitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa Idodi Sekondari. Nakiri kuwa kwa akili zangu timamu, taarifa zote nilizotoa hapo juu ni sahihi na zinanihusu.

Jina …….. sahihi ……..… Tarehe ……..……

TAARIFA YA MZAZI/ MLEZI

Jina la Mzazi/ Mlezi …….
Anwani yake……
Namba ya simu ……..
Kazi anayofanya……
Wilaya/Mji anakofanyia kazi……
Anwani ya kazini……..
Namba ya simu ya kazini …….....

AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi……..MZAZI/MLEZI NAKUBALI / SIKUBALI nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari Idodi. Naahidi kuwa nitawajibika/sitawajibika na kumhimiza mwanangu kuzitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitashiriki/sitashiriki kumhimiza kufuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana/sitashirikiana na uongozi wa shule kumhimiza mwanangu kushirikiana na wanafunzi wenzake katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo na kuwa na nidhamu kwa muda wote atakaokaa Idodi Sekondari. Nitapenda/sitapenda kupata taarifa zote zinazomhusu mwanangu muda wote awapo shuleni ***(futa isiyohusika)***

Jina la mzazi/mlezi……..Sahihi……Tarehe…….

WATU WA KARIBU(KIUHUSIANO/UNDUGU) NA FAMILIA AMBAO UNGEPENDA WAPATE TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/ WALEZI

(i) Jina …… Anwani ……
Namba ya simu…… Kazi anayofanya …….……..
Uhusiano wake na mwanafunzi…….....
(ii) Jina **……**Namba ya simu……..Anwani…….
Namba ya simu…… Kazi anayofanya …….……..……
Uhusiano wake na mwanafunzi…….....

NB; Iwapo anwani ya mmojawapo wa Mzazi/Mlezi au ndugu wa karibu amehama au Amefariki lazima mwanafunzi atoe taarifa na kubadilisha jina na kuandika mtu mwingine ambaye atawajibika kwa mwanafunzi.

Fomu Na -C-

FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI INAYOTAMBULIKA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE.

Mimi (Jina la Mganga) ……..
Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)…….
Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonekana kuwa anayo /hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;

(A) Hali ya Mwili.

(i) Mapigo ya moyo……
(ii) Damu (Haemoglobin)……..…..
(iii) Kundi la Damu (Blood group)…….……...
(iv) Mkojo…….
(v) Haja kubwa…….
(vi) Macho ……
(vii) Masikio …….……..

NB. Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa……..
…….

(B) Magonjwa.

Amewahi /hajawahi au hana magonjwa yafuatayo;

(a) Kifua kikuu (TB)……..…
(b) Kifafa (Epilepsy)……
(c) Shinikizo la damu (BP)……..
(d) Magonjwa ya tumbo ……..
(e) Seli mundu (Sickle cells)…….……
(f) Ukoma……
(g) Magonjwa ya zinaa (taja aina)……
(h) Ugonjwa wa akili ……...…

(i) Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu
….……

Maoni ya Daktari ……..……

Saini na Muhuri wa Daktari/Mganga wa Hospitali ya Serikali.

…….……..

MSANGI, B.H
MKUU WA SHULE